



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Kumb. Na. JA/301/300/06/VOL.1/100

Tarehe: 01/08/2024

**TANGAZO LA KAZI ZA URASIMISHAJI WA MAKAZI YASIYOPANGWA
KATIKA HALIMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE**

1. UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ilianzishwa na kutangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali mwaka 2013. Wilaya ya Nyang'hwale ni moja kati ya Wilaya zinazounda Mkoa wa Geita. Wilaya ya Nyang'hwale ina vitovu vya vijiji vinavyokua kwa kasi kutokana na ongezeko kubwa la ujenzi wa makazi yasiyopangwa. Halmashauri imedhamiria kumaliza makazi holela kwa kufanya urasimishaji kwa maeneo hayo na kupima maeneo yote yaliyoiva kimji.

2. MAENEO YA URASIMISHAJI

Ili kuboresha makazi ambayo hayajapangwa, Halmashauri inatangaza nafasi kwa makampuni ya upangaji na upimaji kuomba kazi za urasimishaji kwa maeneo kumi na moja (11) ambayo yana sifa za kurasimishwa. Maeneo hayo ni **Kharumwa (Bupamba, Nyaweshi, Manyema, Butimwa) Busengwa, Busolwa, Nyijundu, Nyang'hwale** (senta za Nyang'hwale na Nyang'hurukuru), **Bukwimba, kata ya Kakora** katika senta za vijiji vya (**Kakora, Ligembe na Kitongo**)

Makadrio ya viwanja vitakavyorasimishwa

NA.	KIJIJI	IDADI YA VIWANJA TEGEMEWA
1	Kharumwa kitongoji cha Bupamba	1000
2	Kharumwa kitongoji cha Nyaweshi	750
3	Kharumwa kitongoji cha Manyema	500
4	Kharumwa kitongoji cha Butimwa	500
5	Kharumwa kitongoji cha Mahango	750
6	Busengwa	1500
7	Busolwa	1500
8	Nyijundu	1000
9	Kata ya Nyang'hwale (senta za Nyang'hwale na Nyang'hurukuru)	750
10	Kata ya Kakora (senta za Kakora, Ligembe na Kitongo)	750
11	Bukwimba	750
	JUMLA	9,750

3. SIFA ZA KAMPUNI ZINAZOTAKIWA

- i. Kampuni inatakiwa kuwa na mtaji wa kuanzia kazi usiopungua robo ya gharama za mradi kwa eneo utakalopewa.
- ii. Kama inavyoelekezwa katika mwongozo wa urasimishaji makazi yasiyopangwa nchini wa mwaka 2021 ni lazima kampuni ya upangaji inayoomba kazi lazim iwe na makubaliano na kampuni ya upimaji, hivyo hivyo kampuni ya upimaji inayoomba kazi lazima iwe na makubaliano na kampuni ya upangaji.
- iii. Kampuni lazima iwe imesajiliwa na bodi ya kitaaluma yaani Bodi ya Usajili ya Wataalam wa Mipango Miji kama kampuni ni ya upangaji au Halmashauri ya Wapima Ardhi Tanzania kama kampuni ni ya upimaji
- iv. Kampuni lazima iwe na cheti cha usajili kutoka BRELA
- v. Kampuni lazima iwe na ofisi yenye anwani kamili ya mahali ilipo ndani ya nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- vi. Iwe na leseni hai inayoiruhusu kufanya kazi za Mipangomiji au Upimaji nchini;
- vii. Iwe na wataalamu wa kutosha na wenye ujuzi na uwezo sahihi wa fani ya Mipangomiji waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango miji au Halmashauri ya Wapima Ardhi Tanzania watakaofanya kazi za ushauri na za uwandani
- viii. Iwe haidaiwi kodi yoyote na Serikali
- ix. Isiwe na mgongano wa maslahi.
- x. Kampuni iwe na uwezo wa kumaliza kazi ndani ya muda wa miezi mitatu tangu kupewa kazi katika eneo atakalopangiwa

4. JINSI YA KUOMBA

Kampuni binafsi au taasisi iliyo na sifa tajwa hapo juu inakaribishwa kutuma maombi kabla au siku ya ijumaa tarehe **16/08/2024** kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, **S.L.P 352 NYANG'HWALE** kwa barua ya maombi iliyosainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni au yeyote aliyepewa mamlaka na Mkurugenzi Mkuu (Power of Attorney) ikiwa imeambatanishwa na Uzoefu wa kazi za urasimishaji (company profile), Leseni hai vyeti vya usajili wa BRELA na bodi za kitaaluma, hati ya maelezo ya benki (current bank statement) na Uthibitisho wa Malipo ya kodi za serikali

Tangazo hili limetolewa na;



Husna Toni

Mkurugenzi Mtendaji (W)

NYANG'HWALE.

MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
NYANG'HWALE

Nakala:- Mbao za Matangazo na katika Tovuti ya Halmashauri.